# Master plan ya makazi Ruvuma itavyochochea uchumi mkoani

**Na Albano Midelo**

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amezindua 'master plan' yenye mipango kabambe ya Manispaa ya Songea ya mwaka 2017 mpaka 2037 pamoja na ofisi ya ardhi ya Mkoa wa Ruvuma.

Akisoma taarifa ya mpango huo kabambe kwa niaba ya mkurugenzi wa manispaa hiyo, afisa mipangomiji Edward Kandonga alisema kuwa halmashauri ya manispaa hiyo walipitisha azimio la kuandaa *master plan* hiyo kupitia mkutano wa baraza la madiwani uliofanyika Julai 30, 2013.

Alitaja hatua iliyofuata kuwa waliunda kamati ya kitaalam na kamati ndogo kadhaa, pamoja na kutangaza eneo la mpango la zoezi la kukusanya takwimu na kufanya mkutano wa kwanza wa wadau Mei 2014.

Kandonga alisema kuwa mkutano wa pili ilikuwa ni kupendekeza rasimu ya mpango Aprili 19, 2016 kwa wizara yenye dhamana na ardhi pamoja na kuwasilishwa Oktoba 31, 2017, na kwamba hadi Januari 15 mwaka jana 2019 mpango huo uliidhinishwa.

Alisema kuwa sababu iliyosababisha Manispaa ya Songea waandae mpango huo ilikuwa ni kumalizika mpango wa awali ulioandaliwa mwaka 1990, ambao ulikoma mwaka 2010.

"Mpango mpya wa *master plan* umewekwa kulingana na matumizi ya ardhi na kuweka miradi mikubwa ya Manispaa ya Songea, na kuwa na manispaa safi na salama na kukuza uchumi," Kandonga alisema.

Afisamipango miji huyo alisema kuwa katika mpango huo unaoanzia 2017 hadi 2037, yapo maeneo ya matumizi mbalimbali kwenye Manispaa ya Songea, ambayo yametengwa kwa ajili ya viwanda na biashara.

Alitaja maeneo ambako yameandaliwa kwa ajili ya viwanda na biashara kuwa ni kata za Lilambo,Tanga na Mletele.

Alisema kuwa *master plan* hiyo inaonesha matumizi mbalimbali ya ardhi, na kwamba mpango wake imeanza kutekelezwa na halmashauri kwa kupimwa viwanja vinavyoonekana kwenye ramani ambamo kuna maeneo ya viwanda.

***Master plan*** hiyo inaonesha kuwa Kata ya Tanga ni eneo lenye miradi mikubwa inayotekelezwa, ikiwemo kituo kikuu cha ya mabasi Mkoa wa Ruvuma.

Alisema kuwa, katika Kata ya Mletele, kumejengwa kituo kikubwa cha umeme wa gridi ya taifa katika eneo la makazi, wakati pia kuna eneo la biashara na matumizi mbalimbali ya taasisi.

"Mpango huo kabambe mpaka kukamilika umegharimu zaidi ya shilingi milioni 200, na ofisi ya Rais (TAMISEMI) iliratibu mpango huu, na Halmshauri ya Manispaa ya Songea imetekeleza mpango huu," amesema.

Alitaja matarajio ya mpango huo baada ya miaka 20 kuwa ni kuongezeka viwanda vikubwa, viwanda vya kati na viwanda vidogo, pamoja na kuwezesha Manispaa ya Songea iwe kitovu kikubwa cha biashara na kukuza uchumi wa taifa kwa ujumla.

Alisema kuwa uwepo wa maeneo ... lmashauri ya manispaa hiyo, wanatarajia kwamba watakuwepo wawekezaji wengi, ajira zitapatikana kwa ajili ya vijana, ghorofa zitajengwa na mazingira yatahifadhiwa kwenye vyanzo vya maji.

Kwamba, katika awamu ya kwanza ya utekelezwaji wa mpango huo kabambe kuanzia 2017 hadi 2022, itakuwa ni kusambaza uelewa kwa wananchi kuhusu uwepo kwa mpango huo, pamoja na kutoa ardhi kwa miji mitatu ya Lilambo,Tanga na Mletele.

Kuhusu awamu ya pili ya utekelezaji, alisema kuwa itakuwa ya miaka kumi kuanzia mwaka 2020 hadi 2032, ambapo itakuwa ni uwekezaji wa viwanda vidogo, viwanda vikubwa na viwanda vya kati, sanjari na uanzishwaji miundombinu ya barabara.

Alisema kuwa, awamu ya tatu ya utekelezaji mpango huo itakuwa ni miaka mitano kati 2032 hadi 2037, ambayo itakuwa ni uendelezwaji wa eneo la katikati ya mji wa Songea, ambako ni kioo cha Mkoa wa Ruvuma.

Gharama za kuendeleza mpango huo wa *master plan* hiyo ya Manispaa ya Songea ni zaidi ya shilingi trilioni tano, ambazo inatarajiwa zipatikana kupitia vyanzo vya mapato ya ndani vya halmashauri.

Vyanzo vingine ni utekelezaji mpango huo alitaja kuwa ni kutoka serikali kuu, ubia na sektabinafsi, wafadhili yaani Benki ya Dunia (WB), mashirika ya kijamii, TARURA, mamlaka ya viwanja vya ndege, TANROADS, TANESCO na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Songea (SOUWASA).

Kabla ya kuzindua ofisi ya ardhi Mkoa wa Ruvuma, wakazi wa mkoa huo ilikuwa wakisafiri umbali mrefu hadi mkoani Mtwara kufuatilia usajili wa hati za kumiliki ardhi ili wakabidhiwe hatimiliki zao.

Akizindua ofisi hizo, waziri Lukuvi alisema kuwa wananchi watumie ofisi hiyo na wataalamu wake ili kutatua changamoto za migogoro ya ardhi iliyokuwa ikijitokeza kabla.

"Ofisi hii ni yenu wana Ruvuma na wakurugenzi, na mnatakiwa kuitumia ipasavyo. Tutaleta mitambo ya kuskani majalada yenu yaliyotunzwa nyaraka mbalimbali za umilikishaji wa ardhi zote, ili ziingie kwenye mfumo na ramani zote, ziingie kwenye mfumo.

"Tunataka masikini na tajiri wamilikishwe eneo, na serikali ipate kodi," Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi alisema.

**Ofisa mipangomiji ametaja matarajio ya master plan hiyo baada ya miaka 20 kuwa ni kuongezeka viwanda vikubwa, viwanda vya kati na viwanda vidogo, pamoja na kuwezesha Manispaa ya Songea iwe kitovu kikubwa cha biashara na kukuza uchumi wa taifa kwa ujumla ...**

Waziri Luvuki alisema kuwa mwananchi wa kawaida hati yake ikisajiliwa kwenye ofisi ya mkoa, lazima serikali impelekee, na kwamba hata wale wananchi wa vijijini hati zao zimepelekwe kwenye halmashauri zao.

"Nimemuagiza msajili wa hati kwamba mwananchi wa kawaida hati yake ikishatoka Mbinga na imesajiliwa ofisi za mkoa, ni marufuku kwa mwananchi huyo kufuata hati, achukue katika halmashauri yake, ardhi isiwe na usumbufu tena katika kupata hati," alisisitiza.

Alionya wanasheria wanaodanganya wananchi kufuatilia hati zao Mtwara ili wawatapeli fedha zao, sababu Mkoa wa Ruvuma hivi sasa wanatoa huduma hizo, huku akisisitiza kuwa kuanzia mwananchi anapojaza fomu asilipe gharama yoyote.

Alidokeza katika uzinduzi huo kuwa alirudisha nyaraka zote za Mkoa wa Ruvuma zilizokuwepo Mtwara kabla na baada ya uhuru, akisisitiza kwamba kupitia ofisi ya ardhi ya Mkoa wa Ruvuma, sasa wananchi wanaweza kukopesheka na kuongeza mzunguko wa fedha katika kilimo na kukopa benki.



Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi. (Picha ya mtandaoni)

Scanned with CamScanner